



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI



Unapojibutafadhalitaja:

09 Novemba, 2023

Kumb. Na.KMC/LD/161976/JPM

MKURUGENZI MTENDAJI,
KITUO CHA UWEKEZAJI TANZANIA (TIC)
S.L.P, 938,
DAR ES SALAAM.

**YAH: KIWANJA NAMBA 1503/1 ENEO LA MSASANI PENINSULA
MANISPAA YA KINONDONI DAR ES SALAAM.**

Kichwa cha habari hapo juu cha husika na pia rejea barua yako yenye **Kumb Na. CA.148/234/01F/101** ya tarehe 07 Novemba,2023 ikiomba uthibitisho wa umiliki wa kiwanja tajwa.

2. Katika kumbukumbu za ofisi historia inaonyesha kuwa kiwanja namba 1503/1 eneo la Msasani Peninsula awali kilimilikishwa kwa ndugu Hassani Shivji Karim wa S.L.P 4868 Dar es salaam kwa hati namba 44605 ya tarehe 01/04/1995.
3. Aidha, tarehe 21/05/1999 ndugu Hassani Shivji Karim alifanya uhamisho wa miliki hii kwenda kwa ndugu Muslim Shivji Karim wa S.L.P 4868 Dar es Salaam na taratibu za uhamisho wa miliki ulikamilika kwa mujibu wa sheria.
4. Hata hivyo, matumizi ya kiwanja Na. 1503/1 eneo la Msasani Peninsula ni "**Makazi zaidi ya familia moja**" kwa kuzingatia kifungu 'B' kijifungu (b) kama ilivyoainishwa katika sheria ya Mipangomiji Na. 8 ya mwaka 2007, Kifungu 77 (1) (i) (Kanuni ya Vifungu vya matumizi mwaka 2018).
5. Unashauriwa kupata taarifa zaidi katika ofisi ya Kamishana msaidizi wa ardhi wa mkoa wa Dar es salaam pamoja na ofisi ya msajili wa hati.

Ramla A. Mwash
Kny: **MKURUGENZI WA MANISPAA**